



## UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM COMPUTING CENTRE

P. O. Box 35062,  
Dar-Es-Salaam,  
Tanzania.  
Email: [mducc@udsm.ac.tz](mailto:mducc@udsm.ac.tz)

Tel: 255 (22) 2410645  
255 (22) 2410500-8 Ext. 2720  
Mobile: 0754-782120  
Fax: 255 (22) 2410690



### TANGAZO LA KAZI YA MUDA MFUPI

University of Dar Es Salaam Computing Centre (UCC) ilishinda zabuni ya kujenga mfumo, kusambaza vifaa na kutoa huduma ya Uendeshaji wa Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es salaam (DITF), maarufu kama Maoenesho ya Sabasaba yatakayoanza Juni 28 hadi Julai 13, 2022 kwenye viwanja vya Maonesho ya Sabasaba vilivyopo barabara ya Kilwa, Temeke - Dar es Salaam.

Hivyo, UCC inapenda kutangaza nafasi za kazi za muda mfupi kwa ajili ya kushughulikia huduma za uendeshaji wa maonesho na kuuza Tiketi za kuingia uwanjani (watu na magari).

#### SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe mtanzania mwenye Umri usiozidi miaka thelathini (30); ii. Awe na elimu ya kidato cha Sita au Diploma na kuendelea; iii. Awe mwaminifu na mwenye uwezo wa kutunza fedha na vifaa vya kazi; na iv. Awe na udhamini wa mfanyakazi wa University of Dar es salaam (UDSM) au UCC.

#### MAOMBI YAAMBATANISHWE NA NYARAKA ZIFUATAZO:

- i. Barua ya Maombi ya Kazi ii. Nakala ya Cheti cha Kidato cha Sita au Diploma
- iii. Maelezo Binafsi (CV) yakionesha umri, anuani kamili, namba ya simu ya mkononi n.k.
- iv. Picha ndogo (passport size)
- v. Taarifa za mdhamini wako kama vile jina kamili, idara anayofanyia kazi, na namba ya simu ya mkononi.
- vi. Maombi yote yatumwe kwa njia ya **mtandao (Online)** kupitia mfumo wetu wa kielektroniki unaopatikana kupitia <https://jobs.ucc.co.tz/user/register>

Maombi yoyote yatakayowasilishwa kwa njia ya posta au kuletwa moja kwa moja Ofisini hayatafanyiwa kazi.

Mwisho wa kupokea maombi ni **Juni 22, 2022 Saa 5.30 asubuhi**.

Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza.

## MUHIMU:

**Unashauriwa kuweka jina lako kwenye majina ya nyaraka zako**

### **mfano:**

- **juma\_manenge\_photo.png,**
- **juma\_manenge\_f4.pdf,**
- **juma\_manenge\_cert.pdf,**
- **juma\_manenge\_f6.pdf,**
- **juma\_manenge\_dip.pdf**
- **juma\_manenge\_degree.pdf,**
- **juma\_manenge\_letter.pdf,**
- **juma\_manenge\_cv.pdf**

Watakaokidhi vigezo vyote ndio watakaoitwa kwenye usaili. Majina ya watakaochaguliwa (Shortlisted) yatawekwa kwenye tovuti ya UCC  
<https://www.ucc.co.tz>

Barua ya maombi ielekezwe kwa:

Mkurugenzi Mtendaji,  
University of Dar Es Salaam Computing Centre (UCC),  
S.L.P 35062,  
Dar es Salaam, TANZANIA

Tangazo limetolewa na:

**Kaimu Mkurugenzi Mtendaji**

**Juni 17, 2022**

